

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

Simu: +255 (0) 26 2322602

Tovuti: www.maji.go.tz

Barua pepe: ps@maji.go.tz



NBC Tawi la Mazengo,
Barabara ya Kuu,
S. L. P. 456,
40473 Dodoma.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Waziri wa Maji Mhe, Profesa Makame Mbarawa (Mb) amemsimamisha kazi Mhandisi wa Mkoa wa Rukwa, Bi. Emmy George na kumteua Mhandisi Shabani Kassim kukaimu nafasi hiyo kuanzia leo.

Profesa Mbarawa amechukua hatua hiyo baada ya kuukagua Mradi wa Maji wa Isale uliopo katika Wilaya ya Nkasi na kutofurahishwa na maendeleo ya mradi huo, pamoja na maelekezo aliyoyatoa alipofika kwenye mradi huo mwezi Septemba, 2018 na kutoridhishwa na majibu alipotaka ufafanuzi kutoka kwa Mhandisi Emmy George. Bi. Emmy George atapangiwa kazi nyingine.

Aidha, Profesa Mbarawa ameelekeza Mkandarasi wa Kampuni ya Fally Enterprises akamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya dola kwa kosa la udanganyifu wa leseni ya kazi, ambayo haiendani na uwezo wake kitaalamu.

Hatua hiyo imetokana na uchunguzi uliofanyika mara baada ya mkandarasi huyo kuonekana hana uwezo katika kazi anazozifanya na utekelezaji wake miradi ya maji isiyopungua mitano (5) katika maeneo mbalimbali nchini kuwa chini ya kiwango.

Imetolewa na

Kitengo cha Mawasiliano

23 Mei, 2019